# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI (TUICO)

# KATIBA YA CHAMA YA MWAKA-1995

## REKEBISHO LA TANO - 2015

# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI (TUICO)

# KATIBA YA CHAMA YA MWAKA-1995

## REKEBISHO LA TANO - 2015

# TUICO

## KATIBA YA CHAMA YA MWAKA 1995

| | | |
|---|---|---|
| - | Rekebisho la Kwanza | 1996 |
| - | Rekebisho la Pili | 2000 |
| - | Rekebisho la Tatu | 2005 |
| - | Rekebisho la Nne | 2010 |
| - | Rekebisho la Tano | 2015 |

# YALIYOMO

Ukurasa

Tafsiri ya Maneno ........................................ 2

1. **Sura ya Kwanza:** Jina na Imani ........................... 8

2. **Sura ya Pili:** Madhumuni ....................................10

3. **Sura ya Tatu:** Uanachama ..................................12

4. **Sura ya Nne:** Sekta za Chama, Idara na Vitengo........18

5. **Sura ya Tano:** Matawi, Mikoa, Kanda na Taifa............19

6. **Sura ya Sita:** Uchaguzi na Uteuzi wa Viongozi .........20

7. **Sura ya Saba:** Wawakilishi na Matawi ya Chama .....36

8. **Sura ya Nane:** Mkoa ..........................................46

9. **Sura ya Tisa:** Kanda ..........................................50

10. **Sura ya Kumi:** Mkutano Mkuu wa Taifa.....................53

11. **Sura ya Kumi na Moja:** Baraza Kuu ........................58

12. **Sura ya Kumi na Mbili:** Kamati ya Utendaji ya Taifa 63

13. **Sura ya Kumi na Tatu:** Baraza la Wadhamini ............65

14. **Sura ya Kumi na Nne:** Kamati za Makundi Maalumu .....68

15. **Sura ya Kumi na Tano:** Migogoro ya Kikatiba............77

16. **Sura ya Kumi na Sita:** Kuvunjwa au Kuunganishwa Vyama................................78

17. **Sura ya Kumi na Saba:** Majadiliano na Migogoro ya Kikazi...............................79

18. **Sura ya Kumi na Nane:** Mengineyo .........................82

# TAFSIRI YA MANENO

Katika Katiba hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vinginevyo:-

| | |
|---|---|
| **“Ada”** | Maana yake ni malipo ya kila mwezi anayolipia mwanachama kutoka kwenye mshahara wake ili kuchangia mapato ya Chama kwa lengo la kukiwezesha kuendesha shughuli zake za siku hadi siku kwa mujibu wa Katiba. |
| **“Ada ya Huduma”** | Maana yake ni malipo ya kila mwezi anayolipa mfanyakazi ambaye si mwanachama lakini ananufaika na huduma za Chama. |
| **“Akidi”** | Maana yake ni idadi ya wajumbe wanaohitajika ili Kikao/Mkutano uwe halali kufanyika (Koramu). |
| **“Baraza Kuu”** | Maana yake ni Baraza Kuu la Chama ngazi ya Taifa. |
| **“Baraza la Wadhamini”** | Maana yake ni watu/viongozi walioteuliwa na Baraza Kuu la Chama ambao wameaminiwa na Chama ili kukihami Chama na kusimamia rasilimali, fedha na mapato mengine ya Chama kwa niaba ya wanachama na Chama chenyewe. |
| **“Chama”** | Maana yake ni “TANZANIA UNION OF INDUSTRIAL AND COMMERCIAL WORKERS” kwa kifupi TUICO (CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI). |

| | |
|---|---|
| **“Halmashauri ya Tawi”** | Maana yake ni Uongozi wa Chama katika ngazi ya tawi, ambao unajumuisha na kushirikisha wawakilishi wa mahali pa kazi. |
| **“Kamati ya Utendaji”** | Maana yake ni Kikao cha Chama kinachosimamia utekelezaji wa kazi za Chama za siku hadi siku katika ngazi husika ya Chama. |
| **“Kamati za Majadiliano”** | Maana yake ni Kamati zinazoundwa na Chama kwa ajili ya kuendesha Majadiliano na kufunga Mikataba na Waajiri au Jumuiya ya Waajiri kwa niaba ya Chama chini ya usimamizi na Uongozi wa Katibu Mkuu au Mwakilishi wake bila kuathiri au kuingilia shughuli za Halmashauri za Matawi. |
| **“Kanda”** | Maana yake ni ngazi ya tatu ya muundo wa Chama katika utendaji na uongozi inayotokana na mikoa ya Chama katika Kanda husika. |
| **“Kanuni za Chama”** | Maana yake ni taratibu maalumu zinazopitishwa na Baraza Kuu la Chama ili zitumike kufafanua Katiba na utendaji wa shughuli za Chama. |
| **“Katibu”** | Maana yake ni Mtendaji wa shughuli za Chama za siku hadi siku katika ngazi husika ya Chama. |
| **“Katibu Mkuu”** | Maana yake ni Mtendaji na Msemaji Mkuu wa Chama. |

| | |
|---|---|
| **"Katibu Mkuu Msaidizi"** | Maana yake ni Msaidizi wa Katibu Mkuu katika shughuli za Chama. |
| **"Kamati ya Vijana"** | Maana yake ni Chombo kinachoratibu masuala ya vijana kilichoundwa kwa mujibu wa Katiba hii. |
| **"Kamati za Wanawake"** | Maana yake ni chombo kinachoratibu masuala ya Wafanyakazi Wanawake kilichoundwa kwa mujibu wa Katiba hii. |
| **"Kiingilio"** | Maana yake ni malipo ambayo mfanyakazi hulipa anapoamua kujiunga na Chama ili apate kadi ya uanachama. |
| **"Kijana"** | Maana yake ni Mfanyakazi mwenye umri kati ya miaka 18 na 35. |
| **"Kuunganisha Chama"** | Maana yake ni Chama kimoja kuungana na Chama/Vyama vingine na kuunda Chama kipya. |
| **"Kuvunjwa Chama"** | Maana yake ni Chama kuacha/kukoma kufanya shughuli zake. |
| **"Mali za Chama"** | Maana yake ni rasilimali zikiwemo zinazohamishika, zisizohamishika, fedha na mitaji mingine ya Chama. |
| **"Mapato ya Chama"** | Maana yake ni mapato yanayopatikana kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Chama, kama vile ada, viingilio na michango mingine kama Katiba na Kanuni za Chama zinavyoelekeza. |
| **"Mfanyakazi"** | Maana yake ni mtu yeyote aliyeingia katika mkataba wa kuajiriwa kwa mapato ya ujira |

wa siku, wiki au mwezi. Vile vile mfanyakazi ni mtu yeyote aliyejiajiri.

| | |
|---|---|
| **"Michango"** | Maana yake ni malipo maalumu ambayo wanachama/wafanyakazi huombwa na Chama chao kuchangia endapo kuna jambo maalumu limetokea au linataka kutokea ambapo ada za kawaida (za mwezi) haziwezi kukidhi haja hiyo. |
| **"Mkoa"** | Maana yake ni ngazi ya pili ya muundo wa Chama katika utendaji na uongozi inayotokana na matawi yaliyoko katika Mkoa husika. |
| **"Mkuu wa Sekta"** | Maana yake ni Msimamizi wa shughuli za Chama za siku hadi siku katika sekta husika ya Chama. |
| **"Mkutano"** | Maana yake ni mkusanyiko wa wafanyakazi au wanachama wanaotakiwa kufanya Mkutano wa Chama kikatiba. |
| **"Mkutano Mkuu"** | Maana yake ni Kikao Kikuu cha Chama katika ngazi husika ya Chama. |
| **"Mwajiri"** | Maana yake ni mtu, chombo au mamlaka ambayo inamiliki mali au mtaji katika Kampuni, Taasisi, Shirika au Kiwanda na ameajiri watu kwa madhumuni ya kumfanyia kazi na kuwalipa ujira/malipo. |
| **"Mwanachama"** | Maana yake ni mfanyakazi aliyejiunga na Chama na kukubali masharti ya Katiba, kupewa kadi ya uanachama na anayelipa ada kila mwezi. |

| | |
|---|---|
| **“Mwenyekiti”** | Maana yake ni kiongozi aliyechaguliwa na ambaye huongoza mikutano au vikao katika ngazi husika. |
| **“Mwenyekiti wa Taifa”** | Maana yake ndiye kiongozi wa vikao vyote vya Chama ngazi ya Taifa. |
| **“Mwakilishi Wa Chama”** | Maana yake ni kiongozi au mwanachama anayechaguliwa kufanya kazi kwa niaba ya wanachama wenzake katika shughuli mbalimbali za Chama katika ngazi husika. |
| **“Sekta”** | Maana yake ni Sekta za Chama ambazo ni Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri. |
| **“Sekretarieti ya Chama”** | Maana yake ni chombo kinachoratibu kazi za Chama nakutekeleza maamuzi ya vikao vya Chama chini ya usimamizi na maelekezo ya Katibu Mkuu. |
| **“Shirikisho”** | Maana yake ni Muungano wa Vyama Huru vya Wafanyakazi Tanzania. |
| **“Shop steward”** | Maana yake ni Mwakilishi wa Chama ambaye amechaguliwa ili kushughulikia masuala ya wanachama mahali pa kazi. |
| **“Tawi”** | Maana yake ni ngazi ya kwanza ya Chama mahali pa kazi ambapo wanachama wanajumuika kuanzisha uongozi wao wa Chama. |

| | |
|---|---|
| **“Viongozi”** | Maana yake ni wanachama waliochaguliwa na kukabidhiwa majukumu ya kuwaongoza wanachama wenzao katika ngazi husika ya Chama. |
| **“Vikao vya Chama”** | Maana yake ni mkusanyiko wa viongozi/ watendaji wanaokubalika kufanya vikao vya Chama kikatiba. |

# SURA YA KWANZA
# JINA NA IMANI

## 1.1 Jina la Chama

Jina la Chama litakuwa; TANZANIA UNION OF INDUSTRIAL AND COMMERCIAL WORKERS: Kwa kifupi TUICO (CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI).

TUICO ni Chama huru cha wafanyakazi ambacho lengo lake si kujipatia kipato au faida bali kutetea haki, heshima na maslahi ya wanachama wake na wafanyakazi kwa ujumla.

### 1.1.1 Makao Makuu ya Chama

Makao Makuu ya Chama yatakuwa

Mtaa wa Shariff Shamba Ilala,
Plot No. 21 Block C,
S.L.P. 5680,
DAR ES SALAAM.

### 1.1.2 Kujishirikisha hapa Nchini

1.1.2.1 Chama kitajishirikisha na Shirikisho Huru la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania.

1.1.2.2 Chama kitakuwa na uhusiano wa karibu na Vyama vingine vya Wafanyakazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.1.2.3 Chama hakitajishirikisha na Chama chochote cha Siasa.Chama kitaweza kuunga mkono Sera na vitendo vya Chama chochote cha Siasa zenye manufaa kwa wafanyakazi.

### 1.1.3 Kujishirikisha Kimataifa

1.1.3.1 Chama kinaweza kujishirikisha na Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi ya Kimataifa (Global Unions).

1.1.3.2 Chama kinaweza kuwa na uhusiano wa karibu na Vyama vya Wafanyakazi katika nchi mbalimbali.

## 1.2 Imani ya Chama:

Chama kinaamini kuwa:-

(a) Wafanyakazi wote duniani ni sawa.

(b) Kila mfanyakazi ana haki ya kufanya kazi na anastahili malipo kufuatana na kazi hiyo pamoja na kuheshimiwa kama binadamu.

(c) Mshikamano wa wafanyakazi wote duniani ndiyo njia pekee itakayokuza ushirikiano wa karibu kati ya wafanyakazi na vyama vyao katika nchi zote.

(d) Nguvu ya wafanyakazi itatokana na juhudi zao katika kukuza umoja na mshikamano.

(e) Utengano wa aina yoyote kati ya wafanyakazi ni udhaifu.

(f) Kila mfanyakazi atakuwa huru kujiunga na Chama chochote cha siasa atakachopenda.

# SURA YA PILI
# MADHUMUNI

## 2.1 Madhumuni ya Chama yatakuwa kama ifuatavyo:-

2.1.1 Kuboresha na kuendeleza hali nzuri ya wanachama katika maisha yao wakiwa kazini.

2.1.2 Kushirikiana na kujadiliana na waajiri katika kuunda Kamati za Majadiliano na kuanzishwa kwa Mabaraza ya Wafanyakazi ili kudumisha amani mahali pa kazi.

2.1.3 Kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya mwajiri na mwanachama au mwanachama mmoja na mwingine kwa njia ya makubaliano ya amani kila itakapowezekana.

2.1.4 Kujadili, kufunga na kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Hali Bora za Kazi. Aidha kushirikiana na wahusika wengine katika kusimamia utekelezaji wa Tuzo, Kanuni za Utumishi na Sheria nyingine za kazi zitumikazo nchini.

2.1.5 Kushirikiana na kubadilishana ujuzi na Vyama vingine vya Wafanyakazi nchini pamoja na vile vya Kimataifa kwa madhumuni ya:-

(a) Kupata, kutunza na kutoa taarifa au elimu katika masuala muhimu yahusuyo Vyama vya Wafanyakazi.

(b) Kubadilishana ujuzi au taarifa katika masuala yanayohusiana na hali za wafanyakazi na taratibu za kimataifa kuhusu masuala hayo.

2.1.6 Kuwasiliana na Serikali kuhusu haja ya kutunga sheria sahihi za kazi na kuandaa sera nzuri za kuendeleza uchumi na maisha ya jamii.

2.1.7 Kulinda maslahi ya wanachama kwa kuisaidia Serikali ili kuepukana na uandaaji wa sera ambazo hazina manufaa kwa wafanyakazi.

# SURA YA TATU
# UANACHAMA

## 3.1 Wanachama Waanzilishi

3.1.1 Wafanyakazi wote waliokuwa wanachama wa OTTU katika Sekta za Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri kabla ya kuanzishwa Chama hiki watakuwa wanachama waanzilishi wa Chama.

3.1.2 Waliokuwa watendaji wa OTTU wakati wa kuanzishwa kwa Chama nao ni wanachama waanzilishi wa TUICO.

## 3.2 Wanachama Wapya

3.2.1 Wanachama wapya watatokana na wafanyakazi walioajiriwa/waliojiajiri katika Sekta za Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri na shughuli zinazohusiana na sekta hizo.

3.2.2 Wanachama kwa mujibu wa ajira zao ndani ya Chama chenyewe (TUICO).

## 3.3 Uanachama wa Heshima

3.3.1 Waasisi, Wanachama wengine au watu waliojitolea kukiendeleza Chama wakati wa enzi zao, wanaweza kutunukiwa Uanachama wa Heshima.

3.3.2 Uteuzi wa Wanachama wa Heshima utafanywa na Mkutano Mkuu wa Chama Taifa.

3.3.3 Wanachama wa Heshima hawataruhusiwa kupiga kura katika mikutano na vikao vya Chama.

## 3.4 Kujiunga na Chama

Mfanyakazi anayekubali kujiunga na Chama atajaza Hati ya Idhini kama inavyoelekezwa na Sheria za Kazi, Kanuni,Taratibu na Katiba ya Chama, hatimaye kupewa kadi ya Chama.

## 3.5 Kiingilio, Ada na Michango ya Uanachama.

### 3.5.1 Kiingilio

Mwanachama atalipa kiingilio kwa kiwango ambacho kitapangwa na Mkutano Mkuu wa Chama Taifa na atapewa stakabadhi.

### 3.5.2 Ada ya Kila Mwezi

Wanachama watalipa ada yao kila mwezi katika kiwango kitakachopangwa na Mkutano Mkuu wa Chama Taifa kwa utaratibu ufuatao:-

(a) Mwanachama aliyejiajiri/binafsi atalipa ada yake moja kwa moja tawini/mkoani kwake na atapewa stakabadhi.

(b) Mwajiri atakata ada kutoka kwa wanachama na kuziwasilisha kwenye Chama na kupewa stakabadhi ya ada iliyowasilishwa.

### 3.5.3 Michango

Wanachama watakapotakiwa watawajibika kutoa michango maalum itakayopangwa na Kamati ya

Utendaji ya Taifa katika masuala yanayohusiana na migogoro, maendeleo ya wafanyakazi na Chama chenyewe.

### 3.5.4 Mawasilisho

Kiingilio, Ada na Michango yote ya wanachama itawasilishwa Makao Makuu ya Chama au kwenye akaunti ya Benki iliyoidhinishwa na Chama.

## 3.6 Kadi za Uanachama na Uandikishaji.

Kila mwanachama atapewa kadi yenye namba iliyochapishwa ambayo itajazwa jina lake, anuani yake, kazi yake, tarehe ya kujiunga na Chama,Sekta,Mwajiri na maelezo mengine yoyote kama itakavyoelekezwa na Kanuni za Chama au Taratibu za Chama.

## 3.7 Daftari la Kumbukumbu

Baada ya kukubali kujiunga na Chama, maelezo yote ya mwanachama huyo yaliyomo katika kadi ya uanachama yataingizwa katika daftari la kumbukumbu za Chama kwa madhumuni ya kusaidia kuweka kumbukumbu za michango ya wanachama na kumbukumbu hizo zitatakiwa kuwa sahihi kila wakati.

## 3.8 Haki za Mwanachama

Mwanachama yeyote, isipokuwa Mwanachama wa Heshima, atakuwa na haki zifuatazo:-

**3.8.1** Kuwakilishwa na Chama mbele ya mwajiri wake pamoja na kutetewa katika mashauri na migogoro ya kikazi.

**3.8.2** Kujitetea mbele ya vikao mbalimbali vya Chama na haki ya kuomba rufaa katika ngazi za juu za Chama.

**3.8.3** Kushiriki katika uchaguzi wa uongozi wa Chama kwa mujibu wa Katiba, Masharti, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi wa Chama.

**3.8.4** Kupewa taarifa za fedha zilizokaguliwa, mali za Chama na orodha ya wanachama katika ofisi za Chama kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Chama.

## 3.9 Wajibu wa Mwanachama

Kila mwanachama atakuwa na wajibu wa:-

3.9.1 Kulipa kiingilio, ada ya kila mwezi na michango kwa wakati anaotakiwa.

3.9.2 Kuunga mkono na kusaidia kwa vitendo maendeleo ya Chama.

3.9.3 Kuzingatia Katiba,Kanuni za Chama na kuheshimu maamuzi yaliyotokana na vikao.

## 3.10 Kukoma Uanachama.

Mwanachama ambaye itathibitika kuwa hajalipa ada yake kwa miezi sita (6) mfululizo bila sababu atakuwa amekoma uanachama na atapoteza haki za uanachama mpaka hapo atakapo lipa malimbikizo ya ada anazodaiwa.

## 3.11 Kujiuzulu Uanachama

3.11.1 Mwanachama anaweza kujiuzulu uanachama wake kwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja ya maandishi kwa Ofisi ya Chama ngazi ya Mkoa akieleza sababu za kujiuzulu kwake na nakala kupeleka kwenye Tawi kama lipo na kwa Mwajiri wake.

3.11.2 Mtu yeyote ambaye uanachama wake utakoma kwa kujiuzulu katika Chama hatakuwa na haki zozote za uanachama.

## 3.12 Kufukuzwa Uanachama

Mwanachama anaweza kufukuzwa uanachama iwapo:-

3.12.1 Atagundulika kuwa alijipatia uanachama kwa udanganyifu.

3.12.2 Kwa kukosa uaminifu amefuja au kupoteza mali ya Chama.

3.12.3 Amegundulika kuwa ni mwanachama wa Chama kingine cha Wafanyakazi.

3.12.4 Atafanya vitendo vinavyopingana na Katiba na Kanuni za Chama au maamuzi ya vikao halali vya Chama.

3.12.5 Amekosa utii na uaminifu kwa Chama kama vile kukisaliti Chama katika migogoro ya kikazi.

## 3.13 Kukoma kwa Ajira

3.13.1 Mwanachama ambaye ajira yake itakoma mahali pake pa kazi atatoa taarifa kwa Halmashauri

ya Tawi lake au kwa Mwakilishi wa Chama kwa sehemu ya kazi ambayo haina Halmashauri ya Tawi.

3.13.2 Katibu wa Tawi au Mwakilishi atatoa taarifa mara moja kwa Katibu wa Mkoa kabla ya kufutwa kwa Mwanachama huyo katika daftari la kumbukumbu.

3.13.3 Katibu wa Mkoa ndiye atakayeidhinisha kufutwa kwa mwanachama huyo.

## 3.14 Taratibu za kufukuzwa Uanachama

Utaratibu ufuatao utatumika katika kumfukuza mwanachama:-

3.14.1 Halmashauri ya Tawi/Mwakilishi wa Chama atatoa taarifa kwa Kamati ya Utendaji ya Mkoa na kutoa sababu za kutaka mwanachama husika afukuzwe.

3.14.2 Kamati ya Utendaji ya Mkoa itafanya uchunguzi na kutoa taarifa ya maandishi kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa.

3.14.3 Kamati ya Utendaji ya Taifa itamuarifu mwanachama husika kwa maandishi kuhusu uamuzi wake.

3.14.4 Mwanachama atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Baraza Kuu na uamuzi wa Baraza Kuu utakuwa wa mwisho.

# SURA YA NNE
# SEKTA ZA CHAMA, IDARA NA VITENGO

## 4.1 Sekta

Uanachama utagawanyika katika Sekta za Kazi na shughuli zinazohusiana nazo kama ifuatavyo:-

4.1.1 Sekta ya Viwanda.

4.1.2 Sekta ya Biashara.

4.1.3 Sekta ya Taasisi za Fedha.

4.1.4 Sekta ya Huduma na Ushauri.

## 4.2 Idara

Kutakuwa na Idara za Huduma kama zitakavyoundwa na Baraza Kuu.

## 4.3 Vitengo

Kutakuwa na Vitengo vya Huduma kama vitakavyoundwa na Baraza Kuu.

# SURA YA TANO
# MATAWI, MIKOA, KANDA NA TAIFA

## 5.1 Matawi

Chama kitakuwa na matawi mahali pa kazi kama yatakavyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba hii na Sheria za Kazi.

## 5.2 Mikoa

Chama kitakuwa na Ofisi za Mikoa kama zitakavyoanzishwa na Baraza Kuu.

## 5.3 Kanda

Chama kitakuwa na Ofisi za Kanda kama zitakavyoanzishwa na Baraza Kuu.

## 5.4 Taifa

Kutakuwa na Ofisi ya Makao Makuu ya Chama kama ilivyoainishwa katika Katiba hii.

# SURA YA SITA
# UCHAGUZI NA UTEUZI WA VIONGOZI

## 6.1 Sifa za Mgombea Uongozi

Kutakuwa na sifa za mgombea wa uongozi katika Chama kama zinavyofafanuliwa kwenye Masharti, Kanuni, na Taratibu za Uchaguzi wa Chama.

## 6.2 Uchaguzi

6.2.1 Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Taifa, Katibu Mkuu na Viongozi wengine utafanywa kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama. Uchaguzi utafanyika kila baada ya miaka mitano (5).

6.2.2 Uchaguzi wa Chama kwa ngazi mbalimbali utafanyika kwa mujibu wa Katiba ya Chama, Masharti, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi wa Chama.

6.2.3 Mwanachama/wanachama au mtu mwingine, kwa namna yoyote ile hatakuwa na haki ya kuzuia au kupinga kufanyika kwa uchaguzi wa Chama Mahakamani au kwa namna yoyote ile.

6.2.4 Mwanachama au wanachama waliogombea uongozi katika uchaguzi wa ngazi husika, watakuwa na haki ya kupinga matokeo iwapo itaonekana taratibu za uchaguzi zimekiukwa.

## 6.3 Uteuzi

Viongozi na watendaji wengine watateuliwa na Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji ya Taifa, kutokana na mapendekezo yatakayowasilishwa na Katibu Mkuu.

## 6.4 Mwenyekiti wa Taifa

**6.4.1** Kazi za Mwenyekiti wa Taifa, zitakuwa

(a) Kusimamia na kuongoza Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu, Kamati ya Utendaji ya Taifa na Mikutano mingine kama itakavyoamuliwa na Kamati ya Utendaji.

(b) Kusimamia nidhamu katika mikutano anayoongoza.

(c) Kuweka saini katika kumbukumbu za Vikao na Mikutano ya Taifa.

(d) Kupiga kura ya nyongeza endapo idadi ya kura zilizopigwa zimelingana katika mikutano atakayoongoza ikiwa maamuzi yatahitaji kupigiwa kura.

**6.4.2** Endapo Mwenyekiti wa Taifa atakuwa na udhuru wa kumfanya asiweze kuhudhuria Mkutano au Kikao chochote, Mkutano au Kikao kitamchagua mmoja wa wajumbe kuwa Mwenyekiti wa Muda wa mkutano au kikao hicho tu.

**6.4.3** Endapo nafasi ya Mwenyekiti wa Taifa itakuwa wazi kwa sababu yoyote ile kabla ya Kikao cha Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu litamchagua

Mwenyekiti wa Taifa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, kwa kipindi cha uongozi kilichobakia.

## 6.5 Mwenyekiti wa Kanda

6.5.1 Kazi za Mwenyekiti wa Kanda zitakuwa

(a) Kusimamia na kuongoza Mkutano Mkuu wa Kanda, Kamati ya Utendaji ya Kanda na mikutano mingine ambayo Kamati ya Utendaji ya Kanda itakavyoamua.

(b) Kusimamia nidhamu katika mikutano anayoingoza.

(c) Kuweka saini katika kumbukumbu za Vikao na Mikutano ya Kanda.

(d) Kupiga kura ya nyongeza endapo idadi ya kura zilizopigwa zimelingana katika mikutano atakayoongoza ikiwa maamuzi yatahitaji kupigiwa kura.

6.5.2 Endapo Mwenyekiti wa Kanda atakuwa na udhuru wa kumfanya asiweze kuhudhuria Mkutano au Kikao chochote, Mkutano au Kikao kitamchagua mmoja wa wajumbe wake kuwa Mwenyekiti wa Muda wa Mkutano au Kikao hicho tu.

6.5.3 Endapo nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda itakuwa wazi kwa sababu yoyote ile, Mkutano Mkuu wa Kanda utachagua Mwenyekiti wa Kanda kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanda kwa kipindi cha uongozi kilichobaki.

## 6.6 Mwenyekiti wa Mkoa

6.6.1 Kazi za Mwenyekiti wa Mkoa zitakuwa:-

(a) Kusimamia na kuongoza Mkutano Mkuu wa Mkoa na Kamati ya Utendaji ya Mkoa na Mikutano mingine ambayo Kamati ya Utendaji ya Mkoa itakavyoamua.

(b) Kusimamia nidhamu katika mikutano atakayoongoza.

(c) Kuweka saini katika kumbukumbu za Vikao na Mikutano ya Mkoa.

(d) Kupiga kura ya nyongeza endapo idadi ya kura zilizopigwa zimelingana katika mikutano atakayoongoza ikiwa maamuzi yatahitaji kupigiwa kura.

6.6.2 Endapo Mwenyekiti wa Mkoa atakuwa na udhuru wa kumfanya asiweze kuhudhuria Mkutano au Kikao chochote, Mkutano au Kikao kitamchagua mmoja wa wajumbe wake kuwa Mwenyekiti wa Muda wa Mkutano au Kikao hicho tu.

6.6.3 Endapo nafasi ya Mwenyekiti wa Mkoa itakuwa wazi kwa sababu yoyote ile kabla ya kikao cha Mkutano Mkuu wa Mkoa, Kamati ya Utendaji ya Mkoa itachagua Mwenyekiti kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa, kwa kipindi cha uongozi kilichobakia.

## 6.7 Mwenyekiti wa Tawi

6.7.1 Kazi za Mwenyekiti wa Tawi zitakuwa:-

(a) Kuongoza na kusimamia mikutano yote ya Tawi.

(b) Kusimamia nidhamu katika mikutano anayoongoza.

(c) Kuweka saini katika kumbukumbu za Vikao na Mikutano ya Tawi.

(d) Kupiga kura ya nyongeza endapo idadi ya kura zilizopigwa zimelingana katika mikutano atakayoongoza ikiwa maamuzi yatahitaji kupigiwa kura.

(e) Kuhakikisha kuwa Katiba na Kanuni za Chama zinafuatwa na wale wote wanaohusika.

6.7.2 Endapo Mwenyekiti wa Tawi kwa sababu yoyote ile hawezi kuhudhuria Mkutano, Halmashauri ya Tawi itachagua mmoja wa wajumbe wake kuwa Mwenyekiti wa kikao.

6.7.3 Endapo nafasi ya Mwenyekiti wa Tawi itakuwa wazi kwa sababu yoyote ile, Mkutano wa Wanachama Wote utamchagua Mwenyekiti wa Tawi kumalizia kipindi cha uongozi kilichobakia.

## 6.8 Katibu Mkuu wa Chama

6.8.1 Katibu Mkuu ndiye Mtendaji na Msemaji Mkuu wa Chama atakayewajibika katika utekelezaji wa

maamuzi yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji ya Taifa ya Chama.

### 6.8.2 Katibu Mkuu atafanya kazi zifuatazo:-

(a) Atahudhuria Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji ya Taifa,atasaini na kuweka kumbukumbu za vikao na Mikutano hiyo.

(b) Atasimamia sera na kutekeleza shughuli zote za Chama pamoja na maamuzi yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(c) Atatayarisha na kuwasilisha kwenye Kikao cha Kamati ya Utendaji ya TUICO Taifa na Baraza Kuu taarifa za kazi za Chama, fedha na makisio ya Mapato na Matumizi ya Chama ya mwaka.Vilevile atatayarisha na kuwasilisha taarifa za kazi za Chama kwenye kikao cha Mkutano Mkuu wa TUICO Taifa kwa kipindi husika.

(d) Ataweka saini katika hundi zote za malipo ya Chama.

(e) Atawajibika kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa kuhusiana na mapato na matumizi ya fedha za Chama.

(f) Atawajibika kutunza kitabu cha fedha na vitabu vingine vya mahesabu ya

fedha Makao Makuu, kutunza fedha za matumizi ya kila siku, kufanya malipo kwa niaba ya Chama na kutunza nakala zote za stakabadhi za mapato na matumizi.

(g) Atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa Katiba na Kanuni za Chama zinafuatwa na wote wanaohusika.

(h) Ataandaa vikao na mikutano yote ya kitaifa pamoja na mikutano maalum.

(i) Ataongoza Majadiliano ya Pamoja baina ya Chama na Waajiri au Jumuiya za Waajiri na anaweza kukasimu jukumu la kuongoza Majadiliano kwa Viongozi na Watendaji walio chini yake.

(j) Kufunga na kusimamia utekelezaji wa mikataba.

(k) Kuunda, kusimamia na kuratibu Mabaraza ya Wafanyakazi na Kamati za Majadiliano.

(l) Kuongoza, kusimamia na kuratibu vikao na majukumu ya Sekretarieti ya Chama.

(m) Atawasilisha mapendekezo ya majina ya Viongozi, Watendaji na Wanachama wa Heshima kwa Mamlaka husika za uteuzi.

(n) Atasimamia na kuratibu Mkutano wa Matawi ya Wanachama wa TUICO waliopo Zanzibar.

## 6.9 Katibu Mkuu Msaidizi

6.9.1 Kutakuwa na Katibu Mkuu Msaidizi wa Chama.

6.9.2 Kazi za Katibu Mkuu Msaidizi zitakuwa:-

(a) Kumsaidia Katibu Mkuu wa Chama katika utekelezaji wa shughuli za Chama za siku hadi siku kwa mujibu wa Katiba, Kanuni, Taratibu za Chama na maelekezo ya Katibu Mkuu.

(b) Kukaimu nafasi ya Katibu Mkuu wa Chama pale itakapoonekana ipo haja ya kufanya hivyo.

(c) Kusimamia shughuli zote za Kanda na Mikoa.

(d) Kufanya kazi nyingine kama atakavyopangiwa na Katibu Mkuu.

## 6.10 Wakuu wa Sekta

6.10.1 Kutakuwa na Mkuu wa Sekta mmoja katika kila Sekta ya Chama.

6.10.2 Kazi za Mkuu wa Sekta zitakuwa:-

(a) Kusimamia na kuongoza shughuli zote katika Sekta:-

(i) Kujadili, kufunga na kusimamia utekelezaji wa mikataba.

(ii) Kushughulikia migogoro ya kazi katika Sekta.

(iii) Kuendeleza uhusiano bora sehemu za kazi.

(iv) Kuhamasisha Mikoa/kanda na kuingiza wanachama wapya.

(v) Kutunza takwimu na kumbukumbu za wanachama wa Sekta.

(vi) Kusimamia shughuli za afya na usalama.

(vii) Kuhakikisha kuwa wanachama wanapata elimu ya wafanyakazi.

(b) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Ofisi ya Katibu Mkuu.

## 6.11 Katibu wa Kanda

6.11.1 Katibu wa Kanda atakuwa ndiye Mtendaji wa Chama katika Kanda.

6.11.2 Kazi za Katibu wa Kanda zitakuwa:-

(a) Kuhudhuria vikao na mikutano yote ya Chama katika Kanda,atasaini na kutunza kumbukumbu husika.

(b) Kuweka saini katika hundi zote na atawajibika kufanya mawasiliano yote yanayohusika.

(c) Kuandaa na kuwasilisha kwenye kikao cha Kamati ya Utendaji ya Kanda taarifa zote za kazi kwa kipindi husika.

(d) Kutunza vitabu vyote na hati kwa mujibu wa Taratibu na Kanuni za fedha za Chama.

(e) Kuandaa vikao na mikutano yote ya Kanda.

(f) Kuwa Msemaji Mkuu kiutendaji katika masuala ya mikutano ya Chama na shughuli zote katika Kanda.

(g) Kuratibu shughuli zote za Chama katika Kanda na atakuwa kiungo kati ya Mikoa na Taifa.

(h) Kujadili, kufunga na kusimamia utekelezaji wa Mikataba.

(i) Kutunza daftari la Wanachama katika Kanda, na kusimamia uhamasishaji wa mikoa katika kuingiza wanachama wapya.

(j) Kuendeleza uhusiano bora baina ya mikoa katika Kanda.

(k) Kushughulikia masuala ya utafiti, elimu, uimarishaji, Afya na Usalama, na masuala ya kijinsia katika Kanda.

(l) Kuratibu shughuli za Chama, Sera, Sheria na migogoro ya Kazi katika Kanda.

(m) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Ofisi ya Katibu Mkuu.

## 6.12 Katibu wa Mkoa

6.12.2 Katibu wa Mkoa atakuwa ndiye Mtendaji wa Chama katika Mkoa na atafanya kazi kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

6.12.3 Kazi za Katibu wa Mkoa zitakuwa:-

(a) Kuhudhuria vikao na mikutano yote ya Chama katika Mkoa, atasaini na kutunza kumbukumbu husika.

(b) Kuweka saini katika hundi zote na atawajibika kufanya mawasiliano yote yanayohusika.

(c) Kuandaa na kuwasilisha taarifa za kazi za Chama kwenye kikao cha Kamati ya Utendaji ya Mkoa, vilevile ataandaa na kuwasilisha taarifa za kazi kwenye Mkutano Mkuu wa Mkoa kwa kipindi husika.

(d) Kuandaa na kuwasilisha kwa Katibu Mkuu na Katibu wa Kanda taarifa za kazi,makadirio ya mapato na matumizi kwa kipindi husika.

(e) Kutunza vitabu vyote na hati kwa mujibu wa Taratibu na Kanuni za Fedha za Chama.

(f) Kuandaa na kuwasilisha taarifa za kazi kwenye vikao/mikutano ya Mkoa katika kipindi husika.

(g) Kuandaa vikao na mikutano yote katika Mkoa husika.

(h) Kuwa Msemaji Mkuu kiutendaji katika masuala ya mikutano ya Chama na shughuli zote katika Mkoa.

(i) Kukusanya na kupeleka benki fedha zote alizokusanya kutoka kwa wanachama na matawi yote Mkoani mwake na kuwasilisha taarifa ya fedha kwa Kamati ya Utendaji ya Mkoa kila nusu ya mwaka.

(j) Kutuma kwa kila Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa agenda za Mikutano siku kumi na nne (14) kabla ya mikutano kufanyika.

(k) Kuhamasisha na kuingiza wanachama wapya.

(l) Kujadili, kufunga na kusimamia utekelezaji wa Mikataba.

(m) Katibu wa Mkoa atakayekuwa Makao Makuu ya Kanda atafanya shughuli zote za Kanda.

(n) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Ofisi ya Katibu Mkuu.

## 6.13 Katibu wa Tawi

6.13.1 Katibu wa Tawi atakuwa Mtendaji wa kazi za Chama katika Tawi husika na atafanya kazi kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

6.13.2 Kazi za Katibu wa Tawi zitakuwa:-

(a) Kuhamasisha na kuhakikisha kuwa tawi lake linapata wanachama wasiopungua asilimia hamsini (50%) ya wafanyakazi wote.

(b) Kuhudhuria mikutano yote ya Tawi,atasaini na kutunza kumbukumbu za mikutano hiyo na kuwasilisha kumbukumbu hizo kwa katibu wa Mkoa.

(c) Kufanya mawasiliano yote yanayohusika katika Tawi.

(d) Kutunza kumbukumbu za wanachama wote katika Tawi pamoja na tarehe walizojiunga na Chama, nambari za kadi zao na michango ya wanachama.

(e) Kuwasilisha fedha zote alizopokea kwa niaba ya Tawi kwa Katibu wa Mkoa, kila mwezi na kubakiza fungu ambalo limeidhinishwa na Baraza Kuu kubaki Tawini.

(f) Kuandaa taarifa ya kila mwezi itakayoonesha kwa usahihi mapato na matumizi ya Tawi na kuiwasilisha kwenye vikao husika vya tawi na kwa Katibu wa Mkoa.

(g) Kuandaa na kuitisha vikao na mikutano ya kikatiba tawini baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Tawi.

(h) Endapo atajiuzulu au ataacha ukatibu kwa sababu yoyote au atalazimishwa kuacha, atakabidhi kwa Mwenyekiti wa Tawi au viongozi wa Mkoa, fedha zote, vitabu na mali za Chama au mauzo ya mali hizo kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

## 6.14 Kuondoa Uongozi/Kiongozi wa Tawi Madarakani

6.14.2 Iwapo wanachama hawaridhiki na uongozi/ kiongozi wao wa Tawi, na kwa hiyo wana dhamira ya kuuondoa/kumuondoa madarakani, italazimu utaratibu ufuatao utumike:-

(a) Wanachama watapeleka tuhuma zao dhidi ya uongozi/kiongozi wa Tawi kwa Katibu wa Mkoa wa Chama wakiambatanisha majina yao na sahihi zao.

(b) Baada ya Katibu wa Mkoa kupokea tuhuma hizo pamoja na majina ya wanachama na sahihi zao, ataitisha mkutano wa wanachama wote ili kujadili tuhuma hizo, kujiridhisha na kushughulikia usuluhishi kwa njia ya maelewano ndani ya siku kumi na nne (14).

(c) Endapo njia ya usuluhishi imeshindikana Katibu wa Mkoa ataitisha Kamati ya Utendaji ya Mkoa katika muda usiozidi miezi miwili tangu siku ya kushindikana kwa usuluhishi.

(d) Kamati ya Utendaji ya Mkoa itajadili tuhuma hizo kwa kushirikisha uongozi/ kiongozi wa Tawi anayetuhumiwa na wawakilishi wa wanachama na kutolea maoni.

(e) Iwapo maoni ya Kamati ya Utendaji ya Mkoa yameafiki kuondolewa kiongozi/ uongozi wa tawi madarakani, yafuatayo ni lazima yatekelezwe:-

(i) Katibu wa Mkoa wa Chama ataitisha Mkutano wa Wanachama Wote na kura ya kutokuwa na imani na Uongozi/kiongozi wa Tawi itapigwa chini ya usimamizi wa Katibu wa Mkoa.

(ii) Idadi ya kura zinazokubalika kuondoa uongozi/kiongozi wa Tawi madarakani ni theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote.

(f) Katibu wa Mkoa atawasilisha kwa Katibu Mkuu taarifa zifuatazo ndani ya muda usiozidi siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya upigaji wa kura ya kutokuwa na imani kufanyika;

(i) Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Utendaji.

(ii) Matokeo ya kura ya kutokuwa na imani.

(iii) Mahudhurio ya mkutano wa wanachama wote Tawini.

(iv) Orodha ya wanachama wote tawini.

(g) Katibu Mkuu atatoa uamuzi ndani ya kipindi kisichozidi miezi sita tangu apokee taarifa hiyo.

# SURA YA SABA

# WAWAKILISHI NA MATAWI YA CHAMA

## 7.1 Wawakilishi wa Chama sehemu ya kazi (Union Representatives)

7.1.1 Chama kitakuwa na wawakilishi wake mahali pa kazi ambapo wanachama wake wameajiriwa kama ifuatavyo:-

(a) Mahali pa kazi penye mwanachama mmoja mpaka wanachama tisa, mwakilishi mmoja, ambaye atawajibika kwa Katibu wa Mkoa kwa shughuli zote za Chama.

(b) Mahali pa kazi penye wanachama kumi mpaka wanachama ishirini, wawakilishi watatu, angalau mmoja awe mwanamke.

(c) Mahali pa kazi penye wanachama ishirini na mmoja mpaka wanachama mia moja, wawakilishi kumi, angalau watatu wawe Wanawake.

(d) Mahali pa kazi penye wanachama zaidi ya mia moja, wawakilishi kumi na tano, angalau watano wawe wanawake.

7.1.2 Nafasi za uwakilishi wa wanawake zitatolewa tu iwapo wameajiriwa na ni wanachama.

## 7.2 Chama kuanzisha matawi

7.2.1 Chama kitaanzisha matawi mahali pa kazi ambapo wanachama kumi au zaidi wameajiriwa.

7.2.2 Ikiwa wanachama walio chini ya kumi wataridhika kujiunga na wanachama wa mwajiri mwingine ili kuunda Tawi la Mseto, Halmashauri ya Tawi la Mseto litakuwa na Wawakilishi wa kila mahali pa kazi ambapo wanachama wake wamejiunga na Tawi hilo.

7.2.3 Kila tawi litaandikishwa Makao Makuu ya Chama.

7.2.4 Matawi yote ya Chama yana hadhi sawa na yatawajibika kwa Katibu wa Mkoa ambapo Tawi lipo.

## 7.3 Muundo wa Tawi

7.3.1 Halmashauri ya Tawi itaundwa na wawakilishi wa Chama mahali pa kazi na wajumbe wengine watakaochaguliwa kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

7.3.2 Halmashauri ya Tawi itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wajumbe Saba kama Tawi lina Wanachama kuanzia kumi na halina zaidi ya Wanachama ishirini ambao ni:-

(i) Mwenyekiti wa Tawi.

(ii) Katibu wa Tawi.

(iii) Wajumbe watatu wa Tawi angalau mmoja awe mwanamke.

(iv) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake kwenye Tawi.

(v) Katibu wa Kamati ya Wanawake Kwenye Tawi.

(b) Wajumbe kumi na mbili kama Tawi lina zaidi ya Wanachama ishirini na halina zaidi ya wanachama mia moja ambao ni:-

(i) Mwenyekiti wa Tawi.

(ii) Katibu wa Tawi.

(iii) Wajumbe nane wa Tawi angalau watatu wawe wanawake.

(iv) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake kwenye Tawi.

(v) Katibu wa Kamati ya Wanawake Kwenye Tawi.

(c) Wajumbe Kumi na Saba kamaTawi lina zaidi ya wanachama wanaozidi mia moja na wasiozidi elfu moja ambao ni:-

(i) Mwenyekiti wa Tawi.

(ii) Katibu wa Tawi.

(iii) Wajumbe kumi na tatu angalau, watano wawe wanawake.

(iv) Mwenyekiti wa Kamati ya wanawake kwenye Tawi.

(v) Katibu wa Kamati ya Wanawake kwenye Tawi.

(d) Wajumbe ishirini na mbili kama Tawi lina wanachama wanaozidi elfu moja ambao ni:-

(i) Mwenyekiti wa Tawi.

(ii) Katibu wa Tawi.

(iii) Wajumbe kumi na nane angalau, saba wawe wanawake.

(iv) Mwenyekiti Kamati ya wanawake Tawi.

(v) Katibu wa Kamati ya Wanawake Tawi.

7.3.3 Nafasi za ujumbe kwa wanawake zitatolewa tu iwapo wameajiriwa na ni wanachama.

## 7.4 Vikao vya Tawi

Vikao vya tawi vitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Halmashauri ya Tawi.

(b) Mkutano wa Wanachama wote.

(c) Mkutano wa Wafanyakazi wote.

**7.4.1** Halmashauri ya Tawi.

Halmashauri ya Tawi itaitisha mikutano yake angalau mara moja kila baada ya miezi mitatu. Mikutano maalum inaweza ikaitishwa inapobidi.

7.4.1.1 Kazi za Halmashauri ya Tawi na Wawakilishi wa Chama ni kama zifuatazo:-

(a) Kuwawakilisha wanachama mbele ya mwajiri wanapokuwa na malalamiko au wanapokabiliwa na hatua za kinidhamu.

(b) Kulinda na kusimamia haki na maslahi ya wanachama/wafanyakazi, kutoa hoja kwa niaba ya wanachama kuhusiana na Kanuni, Afya na Usalama, Ustawi na kuhakikisha kuwa mazingira ya kazi yanaboreshwa.

(c) Kushauriana na kujadiliana na mwajiri kuhusu mipango ya uzalishaji, kukuza tija, kuendeleza ajira ya haki na kuhakikisha kuwa wanachama wanafaidika kutokana na ziada inayotokana na ongezeko la tija.

(d) Kukiwakilisha Chama kwenye ukaguzi na uchunguzi utakaofanywa na wakaguzi kwa mujibu wa Sheria za Kazi, pamoja na kuhakikisha mwajiri anazingatia Sheria za Kazi.

(e) Kuendeleza uhusiano bora na mwajiri mahali pa kazi.

(f) Kuhamasisha na kuingiza wanachama wapya.

(g) Kuhakikisha wanachama wanatimiza wajibu wao kwa mujibu wa Katiba na haki zao kikatiba zinatekelezwa.

(h) Kupokea, kuwasilisha, kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa maagizo na maelekezo ya ngazi za juu za Chama.

(i) Kutoa taarifa mara kwa mara kwa wanachama kuhusu shughuli za Chama Tawini.

(j) Kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Chama mahali pa kazi kwa Katibu wa Mkoa, ikiwa ni pamoja na taarifa za mambo yanayoweza kusababisha migogoro mahali pa kazi.

(k) Kuendeleza uhusiano bora na matawi mengine.

(l) Kushirikiana na Katibu Mkuu au Mwakilishi wake katika Majadiliano ya Pamoja na Mwajiri.

(m) Kuchagua Wawakilishi (Union Representatives) kutoka miongoni mwao kwa mujibu wa Katiba hii.

(n) Katika matawi makubwa Halmashauri ya Tawi itachagua Wawakilishi (Contact Persons) wenye kazi maalum ya

kuwasiliana na wanachama katika idara au sehemu mbali mbali za mahali pa kazi.

(o) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Tawi na kubuni vyanzo vingine vya mapato.

(p) Kutunza kitabu cha kumbukumbu cha Wanachama.

7.4.1.2 Endapo kunatokea mgogoro wa kikazi unaoweza kusababisha kuzorota kwa kazi, ambapo muafaka umeshindikana kati ya wafanyakazi na mwajiri, Halmashauri ya Tawi itawasilisha mgogoro huo kwa Katibu wa Mkoa kwa hatua zaidi za mgomo.

7.4.1.3 Uamuzi wa kutangaza mgomo utahitaji kibali cha Katibu Mkuu baada ya uamuzi wa Kamati ya Utendaji ya Taifa.

## 7.4.2 Mkutano wa Wanachama wote

Mkutano wa wanachama wote utafanyika kila baada ya miezi sita.

7.4.2.1 Mkutano wa wanachama wote utakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea na kujadili taarifa ya Halmashauri ya Tawi na kuagiza Halmashauri hiyo kutekeleza mambo yatokanayo na taarifa hizo.

(b) Kupokea na kujadili namna ya kutekeleza maamuzi yaliyopitishwa na vikao vya Mkoa, Kanda na Taifa.

(c) Kuwachagua Viongozi wafuatao:-

(i) Mwenyekiti wa Tawi.

(ii) Katibu wa Tawi.

(iii) Halmashauri ya Tawi.

(iv) Wawakilishi katika Mkutano Mkuu wa Mkoa kulingana na idadi ya wanachama katika Tawi.

7.4.2.2 Bila kuathiri yaliyotajwa hapo juu, Halmashauri ya Tawi inaweza kuitisha mkutano wa dharura wa wanachama wote ikibidi.

## 7.4.3 Mkutano wa Wafanyakazi wote

7.4.3.1 Halmashauri ya Tawi itaitisha Mkutano wa Wafanyakazi wote katika Tawi angalau mara moja kwa mwaka na utafanya yafuatayo:-

(a) Kujadili taarifa ya maendeleo ya kazi kama ilivyowasilishwa na mwajiri.

(b) Kujadili taarifa iliyowasilishwa na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi.

(c) Kujadili taarifa iliyowasilishwa na Kamati ya Majadiliano.

(d) Kujadili na kupiga kura ya maoni kuhusu migomo na vitendo vya kupinga.

7.4.3.2 Bila kuathiri yaliyotajwa hapo juu, Halmashauri ya Tawi inaweza kuitisha Mkutano wa dharura wa Wafanyakazi wote ikibidi.

## 7.5 Uchaguzi wa Tawi

7.5.1 Wanachama hai tu ndio watakaoruhusiwa katika Mkutano wa Uchaguzi.

7.5.2 Wanachama hai tu ndio watakuwa na haki ya kupiga kura pamoja na haki ya kuomba uongozi katika tawi au uwakilishi mahali pa kazi.

7.5.3 Mwenyekiti, Katibu, Wajumbe wa Halmashauri ya Tawi na wawakilishi mahali pa kazi, watachaguliwa kila baada ya miaka mitano.

## 7.6 Uchaguzi wa Wawakilishi katika Mkutano Mkuu wa Mkoa

7.6.1 Kila tawi litachagua Wawakilishi katika Mkutano Mkuu wa Mkoa kama ifuatavyo:-

(a) Tawi lenye wanachama zaidi ya 10 lakini wasiozidi 100, mwakilishi mmoja.

(b) Tawi lenye wanachama zaidi ya 100 lakini wasiozidi 500, wawakilishi wawili angalau mmoja awe mwanamke.

(c) Tawi lenye wanachama zaidi ya 500 lakini wasiozidi 1,000, wawakilishi wanne, wawili wawe wanawake.

(d) Tawi lenye wanachama zaidi ya 1,000, wawakilishi sita, angalau watatu wawe wanawake.

7.6.2 Kila sehemu ya kazi yenye Wanachama sita hadi tisa, itachagua mwakilishi mmoja wa Mkutano Mkuu wa Mkoa.

# SURA YA NANE
# MKOA

## 8.1 Vikao vya Chama Ngazi ya Mkoa

Kutakuwa na Vikao vifuatavyo katika Ngazi ya Mkoa:-

(a) Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(b) Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

## 8.2 Mkutano Mkuu wa Mkoa

8.2.1 Mkutano Mkuu wa Mkoa utakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Mkoa.

(b) Katibu wa Mkoa.

(c) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Mkoa.

(d) Wajumbe nane waKamati ya Utendaji ya Mkoa, wawili kutoka kila Sekta.

(e) Wenyeviti wote wa matawi katika Mkoa.

(f) Makatibu wote wa matawi katika Mkoa.

(g) Wajumbe wawakilishi kutoka matawini kulingana na idadi ya wanachama.

(h) Wawakilishi wa Mkoa katika Mikutano ya kanda na Taifa.

(i) Mwakilishi kutoka sehemu ya kazi yenye wanachama sita hadi tisa.

8.2.2. Mkutano Mkuu wa Mkoa ndicho kikao kikuu cha Chama katika Mkoa na utafanyika mara moja katika miaka mitano, inapobidi mikutano maalumu inaweza kuitishwa.

8.2.3 Kazi za Mkutano Mkuu wa Mkoa

8.2.3.1 Mkutano Mkuu wa Mkoa utafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea na kujadili taarifa zilizotolewa na Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

(b) Kutekeleza maazimio yaliyotolewa na vikao vya juu katika Chama.

(c) Kuratibu na kusaidia katika utekelezaji wa shughuli za Chama.

(d) Kujadili na kupendekeza namna ya kuinua hali ya maisha ya wafanyakazi ambao ni wanachama katika Mkoa.

8.2.3.2 Mkutano Mkuu wa Mkoa utachagua viongozi wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Mkoa.

(b) Wajumbe nane wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa, wawili kutoka kila Sekta ya Chama.

(c) Wajumbe watakaowakilisha Mkoa katika Mkutano Mkuu wa Kanda mmoja kutoka kila Sekta ya Chama.

(d) Wajumbe watakaowakilisha Mkoa katika Mkutano Mkuu wa Taifa mmoja kutoka kila Sekta ya Chama.

(e) Wajumbe wawili Vijana kwa kuzingatia jinsia ambao watawakilisha Mkoa katika Mkutano wa Vijana Taifa.

## 8.3 Kamati ya Utendaji ya Mkoa

8.3.1 Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya Mkoa itakayokutana angalau mara moja kila baada ya miezi sita. Kamati hii itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Mkoa.

(b) Katibu wa Mkoa.

(c) Wajumbe nane, wawili kutoka kila sekta.

(d) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake kwenye Mkoa.

8.3.2 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Mkoa

8.3.2.1 Kamati ya Utendaji ya Mkoa itafanya kazi zifuatazo:-

(a) Itapokea na kutekeleza maazimio ya vikao vya juu vya Chama.

(b) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Chama.

(c) Kusaidia matawi katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Chama.

(d) Kupokea na kujadili taarifa iliyotolewa na Katibu wa Mkoa.

# SURA YA TISA
# KANDA

## 9.1 Vikao vya Chama vya Kanda

Kutakuwa na vikao vifuatavyo vya Chama katika Kanda:-

(a) Mkutano Mkuu wa Kanda.

(b) Kamati ya Utendaji ya Kanda.

## 9.2 Mkutano Mkuu wa Kanda

9.2.1 Mkutano Mkuu wa Kanda utakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Kanda.

(b) Katibu wa Kanda.

(c) Wajumbe watano wa Kamati ya Utendaji ya Kanda.

(d) Wenyeviti wa Mikoa katika Kanda.

(e) Makatibu wa Mikoa katika Kanda.

(f) Mjumbe mmoja kutoka kila Sekta ya Chama waliochaguliwa na Mikutano Mikuu ya Mikoa katika Kanda husika.

9.2.2 Mkutano Mkuu wa Kanda ni kikao cha juu cha Chama katika Kanda. Mkutano huu utafanyika mara moja kila mwaka.

### 9.2.3 Kazi za Mkutano Mkuu wa Kanda

9.2.3.1 Mkutano Mkuu wa Kanda utafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za Chama iliyotolewa na Kamati ya Utendaji ya Kanda.

(b) Kutekeleza maazimio yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu wa Chama, Baraza Kuu la Chama na Kamati ya Utendaji ya Chama Taifa.

(c) Kujadili na kupendekeza namna ya kuinua hali bora ya maisha ya wafanyakazi ambao ni wanachama katika Kanda.

9.2.3.2 Mkutano Mkuu wa Kanda utachagua wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Kanda.

(b) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kanda.

## 9.3 Kamati ya Utendaji ya Kanda

9.3.1 Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya Kanda itakayokuwa na wajumbe saba ambao ni:-

(a) Mwenyekiti wa Kanda.

(b) Katibu wa Kanda.

(c) Wajumbe wanne mmoja kutoka kila Sekta

ya Chama.

(d) Mjumbe mmoja mwanamke kutoka Sekta yoyote ya Chama.

9.3.2 Kamati ya Utendaji ya Kanda itafanya kikao mara moja kwa mwaka. Hata hivyo kikao maalumu kinaweza kuitishwa kwa uamuzi wa Kamati hiyo.

### 9.3.3 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Kanda

Kamati ya Utendaji ya Kanda itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea na kutekeleza maamuzi ya vikao vya juu vya Chama.

(b) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kazi za Chama katika Kanda.

(c) Kujadili mapendekezo yaliyotolewa na vikao vya chini vya Chama katika Kanda.

(d) Kujadili taarifa zilizotolewa na Makatibu wa Mikoa wa Kanda hiyo.

# SURA YA KUMI
# MKUTANO MKUU WA TAIFA

## 10.1 Muundo wa Mkutano Mkuu

Mkutano Mkuu wa Taifa ndicho kikao kikuu cha Chama kitakachokuwa na mamlaka ya juu kuliko vikao vyote.

### 10.1.1 Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa

Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na Wajumbe wafuataao:-

(a) Mwenyekiti wa Chama wa Taifa.

(b) Katibu Mkuu wa Chama.

(c) Katibu Mkuu Msaidizi.

(d) Wakuu wa Sekta.

(e) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa.

(f) Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa.

(g) Wajumbe kumi na mbili wa Kamati ya Utendaji ya Taifa watatu kutoka kila Sekta, angalau wanne wawe wanawake, mmoja kutoka kila Sekta.

(h) Wawakilishi wa Sekta toka kila Mkoa.

(i) Wenyeviti wa Kanda.

(j) Wenyeviti wa Mikoa.

(k) Makatibu wa Mikoa.

(l) Wajumbe kumi na mbili wa Baraza Kuu watatu kutoka kila Sekta na angalau wanne wawe wanawake mmoja kutoka kila Sekta.

(m) Wawakilishi wanne kutoka Zanzibar.

## 10.2 Taratibu za Mkutano Mkuu wa Taifa

**10.2.1** Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa utakutana mara moja kila baada ya miaka mitano.

**10.2.2** Mkutano Mkuu Maalumu unaweza kuitishwa na theluthi mbili (2/3) ya Wajumbe wa Baraza Kuu kama kutatokea sababu maalumu. Mkutano Mkuu Maalumu utajadili mambo yale tu yaliyosababishwa kuitishwa kwake.

**10.2.3** Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Taifa itatolewa miezi mitano kabla. Taarifa ya muda mfupi inaweza kutolewa kama itabidi kuitisha Mkutano Mkuu Maalumu.

**10.2.4** Akidi ya Mkutano Mkuu wa Chama itakuwa si chini ya nusu ya wajumbe wote.

**10.2.5** Mwenyekiti wa Taifa ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu wa Taifa. Iwapo kwa sababu zozote zile Mwenyekiti atashindwa kuhudhuria, Mkutano utachagua Mwenyekiti wa Mkutano huo miongoni mwa wajumbe waliohudhuria.

## 10.3 Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa

Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na kazi zifuatazo:-

10.3.1 Kuchagua Viongozi wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Taifa.

(b) Katibu Mkuu.

(c) Wajumbe kumi na mbili wa Baraza Kuu, watatu kutoka kila Sekta angalau wanne wawe wanawake mmoja kutoka kila Sekta.

(d) Wawakilishi wa Chama katika Mkutano Mkuu wa Shirikisho kulingana na Katiba ya Shirikisho.

(e) Wajumbe wa Baraza Kuu la Shirikisho kulingana na Katiba ya Shirikisho.

(f) Mjumbe/wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho kulingana na Katiba ya Shirikisho.

10.3.2 Kupokea, kurekebisha na kupitisha marekebisho ya Katiba ya Chama.

10.3.3 Kuthibitisha, kurekebisha au kufuta uamuzi wowote uliopitishwa na vikao vya chini vya Chama au kiongozi yeyote wa Chama endapo itaonekana inafaa kufanya hivyo.

10.3.4 Kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa za Kazi za Chama za miaka mitano zitakazowasilishwa na Baraza Kuu.

10.3.5 Kupitisha kiwango cha Ada ya Uanachama na Ada ya Uwakala.

10.3.6 Kupokea na kuteua majina ya Wanachama wa Heshima.

## 10.4 Agenda

Mkutano Mkuu Taifa utajadili agenda zilizotayarishwa na Baraza Kuu.

## 10.5 Utaratibu wa Kupiga Kura

Uchaguzi utafanyika kwa kura za siri. Kama nafasi inayogombewa ni moja, mshindi atakuwa yule aliyepata zaidi ya nusu ya kura zilizopigwa, iwapo kura za wagombea zitalingana itabidi uchaguzi urudiwe.

## 10.6 Maamuzi ya Mkutano Mkuu

Maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Chama Taifa yatapitishwa kwa idadi ya zaidi ya nusu ya waliopiga kura kwa kuinua mikono, isipokuwa kama Mkutano Mkuu utaamua vinginevyo.

## 10.7 Marekebisho ya Katiba

Marekebisho yoyote katika Katiba ya Chama yatapitishwa kwa theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa ChamaTaifa.

## 10.8 Hoja na Mapendekezo

10.8.1 Mwanachama binafsi endapo ana hoja binafsi inayohusu shughuli za Chama, atawasilisha hoja hiyo kwanza kwa Katibu wa Tawi, Katibu wa Mkoa, Katibu wa Kanda na kisha Katibu Mkuu wa Chama.

10.8.2 Hoja hiyo ifikishwe Makao Makuu ya Chama miezi mitatu kabla ya Mkutano Mkuu wa Chama Taifa kwa ajili ya kujadiliwa na kupatiwa ufumbuzi.

# SURA YA KUMI NA MOJA
# BARAZA KUU

## 11.1 Muundo wa Baraza Kuu

Wajumbe wa Baraza Kuu watakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Mwenyekitiwa Taifa.

(b) Katibu Mkuu.

(c) Katibu Mkuu Msaidizi.

(d) Wakuuwa Sekta.

(e) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa.

(f) Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa.

(g) Wajumbe kumi na mbili wa Baraza Kuu watatu kutoka kila Sekta angalau wanne wawe wanawake, mmoja kutoka kila Sekta.

(h) Wajumbe kumi na mbili wa Kamati ya Utendaji ya Taifa watatu kutoka kila Sekta, angalau wanne wawe wanawake, mmoja kutoka kila Sekta.

(i) Wenyeviti wa Kanda.

(j) Makatibu wa Kanda.

(k) Wawakilishi wawili kutoka Zanzibar.

## 11.2 Utaratibu wa Vikao vya Baraza Kuu

11.2.1 Baraza Kuu litakutana mara moja kila mwaka.

11.2.2 Kamati ya Utendaji ya Taifa inaweza kuitisha kikao maalumu cha Baraza Kuu. Kikao cha namna hiyo kinaweza kuitishwa vilevile kama theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wa Baraza Kuu la Chama wametaka hivyo kwa maandishi.

11.2.3 Uamuzi wa kuitisha Kikao maalum cha Baraza Kuu utaratibiwa na Katibu Mkuu kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Taifa.

11.2.4 Taarifa na tarehe ya mkutano itatolewa miezi miwili kabla. Taarifa fupi inaweza ikatolewa kwa ajili ya kikao maalumu cha Baraza Kuu.

11.2.5 Mwenyekiti wa Taifa ndiye atakayekuwa Mwenyekiti wa Baraza Kuu. Endapo Mwenyekiti hakuhudhuria kikao, Baraza Kuu litamchagua mmoja wa wajumbe wake kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho.

## 11.2 Kazi za Baraza Kuu

11.2.1 Baraza Kuu litafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kujadili na kupitisha Sera za Chama.

(b) Kujadili mipango ya kazi za Chama, makadirio ya mapato na matumizi kama yalivyotayarishwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(c) Kuhakikisha kwamba shughuli za Kamati ya Utendaji zinaendeshwa kwa mujibu wa Katiba na Kanuni ya Chama.

(d) Kuidhinisha viwango vya mishahara na marupurupu ya watendaji wa Chama.

(e) Kumteua Mkaguzi wa Nje anayetambulika na kumuidhinisha kufanya ukaguzi wa Hesabu za Fedha na Mali za Chama kwa Mwaka husika.

(f) Kupokea, kurekebisha na kupitisha mapendekezo ya:-

i. Kanuni za Katiba ya Chama.

ii. Kanuni za Fedha.

iii. Kanuni za Utumishi.

iv. Masharti, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi.

(j) Kuidhinisha mahusiano na Vyama vya Wafanyakazi kitaifa.

(k) Kuidhinisha mahusiano ya kimataifa pamoja na kujishirikisha na Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi Kimataifa na kutoa taarifa katika Mkutano Mkuu wa Chama Taifa unaofuata.

(l) Kushughulikia na kuamua rufaa zinazoletwa mbele yake kutoka vikao vya chini vinavyohusiana na:-

(i) Masuala ya kinidhamu ya wanachama na viongozi.

(ii) Masuala ya malalamiko yatokanayo na uchaguzi na mambo mengine yoyote yatakayoletwa mbele yake kama rufaa kwa uamuzi.

(m) Kuandaa ajenda za Mkutano Mkuu waTaifa.

(n) Kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa za Kazi za Chama zitakazowasilishwa na Kamati ya Utendaji Taifa.

(o) Kuchagua Wajumbe kumi na mbili wa Kamati ya Utendaji ya Taifa watatu kutoka kila Sekta angalau wanne wawe wanawake mmoja kutoka kila Sekta.

(p) Kuteua Wadhamini wa Chama ngazi ya Taifa.

(q) Kuteua na kuthibitisha Katibu Mkuu Msaidizi, Wakuu wa Sekta na Makatibu wa Kanda.

(r) Kuthibitisha kuundwa kwa Mikoa, Kanda, Idara na Vitengo vya Huduma za Chama na Kamati za makundi maalumu ndani ya Chama.

(s) Kupokea na kupitisha majina ya waasisi, wanachama waliostaafu na watu wengine waliojitolea kukiendeleza Chama wakati wa enzi zao kwa ajili ya kutunukiwa Uanachama wa Heshima na Mkutano Mkuu.

(t) Kupitia upya maamuzi yake ya uteuzi na wanaweza kutengua pale itakapoonekana inafaa kufanya hivyo kama itakavyowasilishwa na Katibu Mkuu.

## 11.4 Agenda

Baraza Kuu litajadili agenda zilizotayarishwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

# SURA YA KUMI NA MBILI
# KAMATI YA UTENDAJI YA TAIFA

## 12.1 Muundo wa Kamati ya Utendaji ya Taifa

Kamati ya Utendaji ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Taifa.

(b) Katibu Mkuu.

(c) Katibu Mkuu Msaidizi.

(d) Wakuu wa Sekta.

(d) Wajumbe kumi na mbili wa Kamati ya Utendaji ya Taifa.

## 12.3 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Taifa

12.3.1 Kazi za Kamati ya Utendaji ya Taifa zitakuwa:-

(a) Kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa za Kazi za Chama zitakazowasilishwa na Katibu Mkuu.

(b) Kupokea na kupitia Kanuni za Chama.

(c) Kusimamia utekelezaji wa kazi za Chama.

(d) Kuteua na kuajiri, Wakuu wa Idara, Vitengo na Makatibu wa Mikoa.

(e) Kupokea na kupitia maandalizi ya vikao vya Baraza Kuu na Mkutano Mkuu Taifa.

(f) Kudhibiti miiko na maadili ya wanachama na viongozi.

(g) Kushughulikia rufaa za uchaguzi zinazotokana na ngazi ya Kanda.

(h) Kupitia upya maamuzi yake ya uteuzi na wanaweza kutengua pale itakapoonekana inafaa kufanya hivyo kama itakavyowasilishwa na Katibu Mkuu.

(i) Kazi nyingine kama itakavyoagizwa na Baraza Kuu.

12.3.2 Kamati ya Utendaji Taifa itahakikisha kwamba mwenendo wote wa shughuli na kazi za Chama unafuata Katiba na Kanuni za Chama.

## 12.4 Vikao

Kamati ya Utendaji ya Taifa itakutana mara moja kila baada ya miezi sita. Kikao cha dharura kinaweza kuitishwa endapo itatokea haja ya kufanya hivyo.

# SURA YA KUMI NA TATU
# BARAZA LA WADHAMINI

## 13.1 Muundo wa Baraza la Wadhamini

13.1.1 Baraza la Wadhamini litakuwa na Wajumbe wanne ambao watachaguliwa kutoka nje ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji na Baraza Kuu.

13.1.2 Katibu Mkuu atapendekeza majina ya Wadhamini kwa Baraza Kuu kwa ajili ya uteuzi.

13.1.3 Sifa za Wadhamini zitakuwa zifuatazo:-

(a) Wawe na uzoefu wa shughuli za Vyama vya Wafanyakazi.

(b) Wawe wanachama.

(c) Wasiwe watumishi au viongozi watendaji katika Chama.

(d) Wawe tayari kusimama Mahakamani kwa niaba ya Chama.

(e) Wawe na uwezo wa kukihami Chama wakati kinakabiliwa na ukata.

(f) Wawe waadilifu na waaminifu.

13.2 Mali na Raslimali za Chama zitawekwa chini ya usimamizi wa Baraza la Wadhamini.

13.3 Mdhamini atakuwa ameondolewa katika shughuli zake na nafasi yake kuwa wazi iwapo:-

(a) Atafariki.

(b) Atajiuzulu.

(c) Atafilisika.

(d) Atakuwa na akili zisizo timamu.

(e) Atakosa uaminifu.

(f) Atapatikana na kosa la jinai.

(g) Kukaa nje ya nchi kwa muda unaozidi mwaka mmoja.

13.4 Mdhamini anaweza kujiuzulu kwa hiari kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Katibu Mkuu wa Chama miezi miwili kabla ya kujiuzulu kwake.

13.5 Kama itatokea Mdhamini kufariki, kujiuzulu au kuondolewa katika madaraka hayo, nafasi hiyo itajazwa na mdhamini mwingine atakayeteuliwa na Baraza Kuu.

13.6 Hati zote za kumiliki mali inayoondosheka na isiyoondosheka na hati nyingine zozote za Chama zitakuwa tayari kutazamwa na Wadhamini kila watakapotaka kufanya hivyo.

13.7 Hati zote zinazohusiana na miliki ya mali zitakuwa zinatunzwa na Katibu Mkuu ambaye atazitoa kwa Wadhamini kila watakapozihitaji.

13.8 Mdhamini aliyejiuzulu au kuondolewa katika nafasi hiyo kwa sababu zozote atawajibika kukabidhi kwa maandishi

hati za mali zote za Chama alizochukua kwa Katibu Mkuu.

13.9 Suala la uwekezaji rasilimali litaamuliwa na Baraza Kuu. Mdhamini haruhusiwi kuweka rehani mali ya Chama kwa udhamini wa shughuli zake binafsi kinyume na Katiba na Kanuni za Chama.

# SURA YA KUMI NA NNE
# KAMATI ZA MAKUNDI MAALUMU

Kutakuwa na Kamati za Makundi Maalumu ya wanachama ndani ya Chama kama zitakavyoanzishwa na Baraza Kuu.

## 14.1 Kamati za Wanawake

Kutakuwa na Kamati za Wanawake zitakazoundwa katika ngazi za Chama ambazo ni Tawi, Mkoa na Taifa. Wajumbe wa Kamati hizo watachaguliwa katika mikutano ya uchaguzi katika ngazi husika.

Kamati zitawajibika kwa mamlaka husika za Chama.

### 14.1.1 Muundo wa Kamati za Wanawake sehemu ya kazi

(a) Mwakilishi wa Wanawake

(i) Mahali pa kazi penye wanachama wanawake sita mpaka tisa Mwakilishi mmoja.

(ii) Mwakilishi atafanya shughuli zake chini ya usimamizi wa Katibu wa Mkoa.

**(b) Ngazi ya Tawi**

Mahali pa kazi penye wanachama wanawake kumi au zaidi, Wajumbe wa Kamati ya Wanawake watakuwa watano ambao ni:-

(i) Mwenyekiti.

(ii) Katibu.

(iii) Wajumbe watatu.

**14.1.2 Kazi za Kamati za Wanawake Ngazi ya Tawi**

(a) Kusimamia na kusaidia utekelezaji wa shughuli za Wanawake Ngazi ya Tawi.

(b) Kuandaa mapendekezo na maoni ya kuwasilisha katika vikao vya Halmashauri ya Tawi.

(c) Kuhamasisha wafanyakazi wanawake kujiunga na kushiriki katika shughuli za Chama.

(d) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wanawake wa kujiamini na kujitegemea.

(e) Kupigania kuondoa ubaguzi dhidi ya Wanawake ili kuwezesha upatikanaji wa haki za Wafanyakazi Wanawake mahala pa kazi.

(f) Kushauri Chama katika kubuni sera na mikakati ya kuwaendeleza wafanyakazi wanawake.

**14.1.3** Kamati ya Wanawake Ngazi ya Tawi itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu.

**14.1.4** Mkutano wa Wanachama Wanawake ngazi ya Tawi utafanyika mara moja kila baada ya miaka mitano kwa ajili ya Uchaguzi.

### 14.1.5 Muundo wa Kamati za Wanawake Ngazi ya Mkoa

Wajumbe wa Kamati ya Wanawake ngazi ya Mkoa watakuwa kumi ambao ni:-

i. Mwenyekiti.

ii. Katibu wa Mkoa.

iii. Wajumbe wawili kutoka kila Sekta ya Chama.

### 14.1.6 Kazi za Kamati za Wanawake Ngazi ya Mkoa

(a) Kusimamia na kusaidia utekelezaji wa shughuli za Wanawake Ngazi ya Mkoa.

(b) Kuandaa mapendekezo na maoni ya kuwasilisha katika vikao vya Kamati ya Utendaji Mkoa.

(c) Kuhamasisha wafanyakazi wanawake kujiunga na kushiriki katika shughuli za Chama.

(d) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wanawake wa kujiamini na kujitegemea.

(e) Kupigania kuondoa ubaguzi dhidi ya Wanawake ili kuwezesha upatikanaji wa

haki za Wafanyakazi Wanawake mahala pa kazi.

(f) Kushauri Chama katika kubuni sera na mikakati ya kuwaendeleza wafanyakazi wanawake.

**14.1.7** Kamati ya Wanawake Ngazi ya Mkoa itakutana mara moja kila baada ya miezi sita.

**14.1.8 Mkutano wa Wanachama Wanawake Ngazi ya Mkoa**

Mkutano wa Wanachama Wanawake Ngazi ya Mkoa utakuwa na Wajumbe wafuataao:-

i. Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Mkoa.

ii. Katibu wa Mkoa.

iii. Wenyeviti wa Kamati za Wanawake Ngazi ya Tawi.

iv. Mwakilishi mmoja wa wanawake kutoka mahali pa kazi penye Wanachama wanawake sita mpaka tisa.

**14.1.9 Kazi za Mkutano wa Wanachama Wanawake Ngazi ya Mkoa**

Mkutano wa Wanachama Wanawake Mkoa utachagua wafuatao:

i. Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake kwenye Mkoa.

ii. Wajumbe nane, wawili kutoka kila Sekta ya Chama.

14.1.10 Mkutano wa Wanachama Wanawake Mkoa utakutana mara moja kila baada ya miaka mitano.

**14.1.11 Muundo wa Kamati ya Wanawake Ngazi ya Taifa**

Wajumbe wa Kamati ya Wanawake Ngazi ya Taifa watakuwa kumi ambao ni:-

i. Mwenyekiti.

ii. Katibu Mkuu.

iii. Wajumbe nane, wawili kutoka kila Sekta ya Chama.

**14.1.12. Kazi za Kamati ya Wanawake Ngazi ya Taifa**

(a) Kusimamia na kusaidia utekelezaji wa shughuli za Wanawake Ngazi ya Taifa.

(b) Kuandaa mapendekezo na maoni ya kuwasilisha katika vikao vya Kamati ya Utendaji Taifa.

(c) Kuhamasisha wafanyakazi wanawake kujiunga na kushiriki katika shughuli za Chama.

(d) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wanawake wa kujiamini na kujitegemea.

(e) Kupigania kuondoa ubaguzi dhidi ya

Wanawake ili kuwezesha upatikanaji wa haki za Wafanyakazi Wanawake mahala pa kazi.

(f) Kushauri Chama katika kubuni sera na mikakati ya kuwaendeleza wafanyakazi wanawake.

14.1.13 Kamati ya Wanawake Ngazi ya Taifa itakutana mara moja kila baada ya miezi sita.

**14.1.14 Mkutano wa Wanachama Wanawake Ngazi ya Taifa.**

Wajumbe wa Mkutano wa Wanachama Wanawake Ngazi ya Taifa ni wafuatao:-

i. Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa.

ii. Katibu Mkuu.

iii. Wenyeviti wa Kamati za Wanawake za Mikoa.

iv. Mwakilishi mmoja wa Mkutano wa wanawake Taifa kutoka kila Mkoa.

v. Makatibu wa Mikoa.

**14.1.15 Kazi za Mkutano wa Wanachama Wanawake Taifa**

Mkutano wa Wanachama Wanawake Taifa utachagua wafuatao:-

i. Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa.

ii. Wajumbe nane, wawili kutoka kila Sekta ya Chama.

14.1.16 Mkutano wa Wanachama Wanawake ngazi ya Taifa utafanyika mara moja kila baada ya miaka mitano kwa ajili ya Uchaguzi.

14.1.17 Mwenyekiti wa Mkutano wa Wanachama Wanawake Taifa atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa. Iwapo kwa sababu zozote zile Mwenyekiti atashindwa kuhudhuria, Wajumbe watamchagua Mwenyekiti wa Mkutano huo miongoni mwa wajumbe waliohudhuria.

## 14.2 KAMATI YA VIJANA

Kutakuwa na Kamati ya Vijana itakayoundwa katika ngazi ya Chama Taifa, ambayo itawajibika katika Ofisi ya Katibu Mkuu wa Chama.

**14.2.1** Kamati ya Vijana Taifa itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana.

(b) Katibu Mkuu.

(c) Wajumbe nane, wawili kutoka katika kila Sekta ya Chama kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

14.2.2 Kamati ya Vijana Taifa itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Kusimamia na kusaidia utekelezaji wa shughuli za Vijana.

(b) Kuandaa mapendekezo na maoni ya kuwasilisha katika vikao vya juu vya Chama.

(c) Kutoa ushauri kuhusiana na uhamasishaji wa vijana, mafunzo na elimu katika Chama.

(d) Kupigania ongezeko la Ajira zenye Staha na mazingira mazuri ya kazi kwa vijana.

(e) Kubainisha mahitaji na changamoto za Vijana.

(f) Kutekeleza Sera na shughuli zifaazo katika kuleta ufanisi ndani ya Chama.

(g) Kuimarisha ushiriki wa Vijana katika vyombo vya maamuzi mahala pa kazi na kuwajengea uwezo wa kujiamini na kujitegemea.

(h) Kupigania kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya Vijana ili kuhakikisha kuwa haki na maslahi yao yanalindwa.

(i) Kuwahamasisha vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli za Chama ikiwa ni pamoja na kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa Katiba hii.

14.2.3 Kamati ya Vijana Taifa itakutana mara moja kila mwaka.

**14.2.4 Mkutano wa Vijana**

**Mkutano wa Vijana utakuwa na wajumbe wafuataao:-**

i) Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana.

ii) Katibu Mkuu.

iii) Wajumbe wanane wa Kamati ya Vijana.

iv) Wawakilishi wawili kutoka katika kila Mkoa wa Chama kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

14.2.5 Mkutano wa Vijana utafanyika mara moja kila baada ya miaka mitano kwa ajili ya Uchaguzi.

14.2.6 Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana ndiye atakuwa Mwenyekiti wa Vikao na Mkutano wa Vijana. Iwapo kwa sababu zozote zile Mwenyekiti atashindwa kuhudhuria, Wajumbe watamchagua Mwenyekiti wa Kikao/Mkutano huo kutoka miongoni mwa wajumbe waliohudhuria.

# SURA YA KUMI NA TANO
# MIGOGORO YA KIKATIBA

15.1 Utata utakaojitokeza kuhusiana na tafsiri ya Katiba, utapelekwa kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa kwa ufafanuzi.

15.2 Mgogoro wowote kati ya TUICO na Chama shiriki cha Shirikisho, utapelekwa kwenye Kamati ya Utendaji ya Shirikisho kwa usuluhishi.

# SURA YA KUMI NA SITA
# KUVUNJWA AU KUUNGANISHWA VYAMA

16.1 Chama kinaweza kuacha kufanya shughuli zake na kuvunjwa kama pendekezo litapitishwa kwa theluthi mbili (2/3) ya wanachama wote na mali yote itakabidhiwa kwa Wadhamini wa Chama TUICO Taifa kwa hifadhi.

16.2 Chama kinaweza kuamua kuvunjwa baada ya uamuzi wa kutaka kuungana na Chama kingine. Uamuzi wa kuungana na Chama kingine utaamuliwa na Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa. Uamuzi huo utapitishwa kwa zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Taifa.

16.3 Iwapo Chama kitavunjwa au kuungana na Chama kingine mali na madeni ya Chama hiki yatachukuliwa na Chama kipya.

# SURA YA KUMI NA SABA
# MAJADILIANO NA MIGOGORO YA KIKAZI

## 17.1 Sera ya Ujumla

(a) Kamati ya Utendaji ya Taifa itawajibika kwa maazimio yanayotokana na migogoro ya kikazi na itakasimu madaraka yake kwa Katibu Mkuu.

(b) Mikataba yote itakayofungwa kutokana na majadiliano ya pamoja ni mali ya Chama na wakati wote lazima iongozwe au kufungwa na Katibu Mkuu au Mwakilishi wake na kushirikisha Kamati husika za Majadiliano.

## 17.2 Kamati za Majadiliano

17.2.1. Kamati za Majadiliano za Chama zitaundwa kwa ajili ya kuendesha Majadiliano nakuingia Mikataba ya pamoja na waajiri au jumuiya ya waajiri kwa niaba ya Chama kwa kuzingatia utaratibu.

### 17.2.2 Utaratibu wa Kuunda na Kuongoza Kamati za Majadiliano

Kamati za Majadiliano za pande mbili au tatu kitaifa zinaweza kuanzishwa iwapo:-

(a) Mwajiri atakuwa na sehemu za kazi zenye matawi zaidi ya moja.

(b) Kamati za Majadiliano zitahusisha Sekta nzima ya kikazi katika kuundwa kwake, ni lazima matawi husika yahusishwe.

(c) Kamati hizi kila mara lazima ziongozwe na Katibu Mkuu au Mwakilishi wake.

**17.2.3 Kazi za Kamati za Majadiliano**

Kamati za Majadiliano zitafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kuandaa rasimu ya Mkataba wa Hali Bora na kuwasilisha kwa Mwajiri chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu wa Chama au Mwakilishi wake.

(b) Kujadiliana na Mwajiri chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu wa Chama au Mwakilishi wake.

(c) Kufunga Mkataba wa Hali Bora kati ya Chama na Mwajiri husika chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu au Mwakilishi wake.

(d) Kutoa taarifa kwa wanachama kuhusu matokeo ya majadiliano kati ya mwajiri na Chama.

**17.2.4. Ukomo wa Kamati za Majadiliano**

Kamati za Majadiliano zitafanya kazi kwa muda usiozidi miaka mitano.

## 17.3 Migomo

17.3.1 Endapo kutatokea haja ya kuitisha mgomo, kura ya maoni itapigwa na wafanyakazi katika tawi hilo. Kiwango cha zaidi ya asilimia hamsini ya

kura za wafanyakazi waliohudhuria Mkutano huo wa kura ya maoni kitahitajika kukidhi masharti ya kuitisha mgomo.

17.3.2 Iwapo mgomo utaitishwa kwa mwajiri mmoja, Katibu Mkuu baada ya kupata kibali cha Kamati ya Utendaji Taifa ataitisha mgomo wa upili kwa mwajiri mwingine ili kudumisha mshikamano ndani ya Chama na kumshinikiza mwajiri wa kwanza atatue mgomo uliosababisha mgomo wa kwanza.

## 17.4 Kitendo cha Kupinga (Protest Action)

17.4.1 Endapo kutatokea haja ya kuitisha kitendo cha kupinga, Kamati ya Utendaji Taifa itatoa idhini kwa Katibu Mkuu kuchukua hatua za kuitisha kitendo cha kupinga kwa kushirikiana na wadau wote.

17.4.2 Endapo Shirikisho au Chama Shiriki kitaitisha kitendo cha kupinga na kuomba ushiriki wa Chama ili kudumisha mshikamano ndani ya Shirikisho au baina ya Vyama Shiriki, Katibu Mkuu atawasiliana na Kamati ya Utendaji Taifa kwa uamuzi.

## 17.5 Mfuko Maalumu wa Mgomo

Kutakuwepo Mfuko Maalumu wa Mgomo kama utakavyofafanuliwa na Kanuni za Chama.

# SURA YA KUMI NA NANE
# MENGINEYO

## 18.1 Akidi (Quorum) ya Mikutano

Bila kuathiri yaliyomo katika baadhi ya vifungu vya Katiba hii, kiwango cha mahudhurio kwa mikutano yote ya Chama itakuwa si chini ya nusu ya wajumbe wanaotakiwa kuhudhuria Mkutano huo.

## 18.2 Kujaza Nafasi zilizo wazi

18.2.1 Kila nafasi itakapoachwa wazi katika Chama, kikao kinachohusika kitaijaza nafasi hiyo mapema iwezekanavyo kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.

18.2.2 Endapo Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa kwa sababu zilizo nje ya uwezo au zile zilizoelezwa na Katiba na Kanuni ya Chama watapungua hadi kutokidhi akidi ya vikao (Quorum) nafasi hizo zitajazwa kwa utaratibu ufuatao:-

(a) Nafasi zilizoachwa wazi zitatangazwa kwa kufuata Masharti, Kanuni na Taratibu za Uchaguzi wa Chama.

(b) Wanachama kutoka sekta ambayo nafasi ya mwakilishi/wawakilishi wake kwenye Kamati ya Utendaji ya Mkoa ipo wazi ndio watakaoshiriki kugombea kujaza nafasi hiyo/hizo.

(c) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa kutoka sekta hiyo watakutana na kufanya uchaguzi wa kujaza nafasi kwa wale walioomba kutoka sekta husika.

(d) Watakaochaguliwa watakuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa kwa kipindi cha uongozi kilichobakia.

18.2.3 Nafasi itakuwa wazi iwapo yafuatayo yatatokea:-

(a) Kuhama chama.

(b) Kufukuzwa kutoka Chama.

(c) Kuacha, kuachishwa kazi au kustaafu kazi.

(d) Kukosa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo bila taarifa.

(e) Uhamisho.

(f) Kifo.

(g) kujiuzulu.

## 18.3 Kujiuzulu

Kiongozi wa Chama anayetaka kujiuzulu anaweza kufanya hivyo kwa kuandika barua kwa Katibu wa kikao kilichomchagua au kama aliteuliwa, kwa kupeleka barua hiyo kwa mamlaka iliyomteua.

## 18.4 Miiko, Maadili na Mamlaka ya Udhibiti.

### 18.4.1 Miiko

**(a) Miiko ya Viongozi wa TUICO**

Viongozi wa Chama hawaruhusiwi kuwa na wadhifa katika Chama cha Siasa au Serikali ambao unaweza kuzua mgogoro wa kimaslahi.

**(b) Miiko ya Watendaji**

Watendaji wote wa Chama watajitolea kukitumikia Chama na hawatajiingiza katika madaraka mengine nje ya Chama bila ya ridhaa ya Kamati ya Utendaji, (nafasi hiyo iwe ya kuchaguliwa, kuteuliwa au kuajiriwa).

**(c) Miiko ya Wanachama**

Mwanachama yeyote haruhusiwi kusimamisha uchaguzi Mahakamani au kupeleka Mahakamani malalamiko au rufaa inayohusiana na uchaguzi wa viongozi wa Chama au utekelezaji wa Katiba, Kanuni za Katiba ya Chama, Masharti, Kanuni au Taratibu za Uchaguzi, kabla ya hatua zote za kushughulikia malalamiko ya rufaa ndani ya Chama kukamilika. Mwanachama atakayekiuka miiko hii atasimamishwa uanachama wake mara moja.

### 18.4.2 Maadili

Maadili ya Viongozi, Watendaji na Wanachama wa TUICO ni:-

(a) Kulinda na kutetea Katiba na Kanuni za Chama.

(b) Kuunga mkono kwa kauli na vitendo juhudi za kuendeleza Chama.

(c) Kuwa muwazi, mkweli na muaminifu.

(d) Kuheshimu maamuzina kutunza siri za Vikao na Mikutano kama inavyoelekezwa na Kanuni za Katiba ya Chama.

### 18.4.3 Mamlaka ya kudhibiti Miiko na Maadili ya Wanachama na Viongozi

Kamati ya Utendaji ya Taifa ndiyo mamlaka ya kudhibiti miiko, mienendo na maadili ya wanachama na viongozi kwa mujibu wa Katiba ya Chama.

## 18.5 Kusimamishwa Uongozi

18.5.1 Kiongozi yeyote wa kuchaguliwa atakayefanya mambo kinyume cha Katiba na Kanuni za Chama atasimamishwa uongozi.

18.5.2 Kamati ya Utendaji ya Mkoa itakuwa na uwezo wa kusimamisha uongozi au viongozi wa kuchaguliwa ngazi ya tawi, lakini watakuwa na haki ya kuomba rufaa kwa Katibu Mkuu. Bila

kuathiri maelezo hayo, uamuzi wa kusimamishwa na Kamati ya Utendaji ya Mkoa, utakuwa na nguvu na utatekelezwa mara moja mpaka Katibu Mkuu atakapoamua vinginevyo.

18.5.3 Kamati ya Utendaji ya Kanda itakuwa na uwezo wa kusimamisha uongozi/kiongozi wa kuchaguliwa ngazi ya Mkoa lakini watakuwa na haki ya kukata rufaa Kamati ya Utendaji ya Taifa.

18.5.4 Bila kuathiri maelezo hayo,uamuzi wa kusimamishwa na Kamati ya Utendaji ya Kanda utakuwa na nguvu na utatekelezwa mara moja hadi pale Kamati ya Utendaji ya Taifa itakavyoamua vinginevyo.

18.5.5 Viongozi waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa na wajumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa watasimamishwa uongozi na Baraza Kuu la Chama, baada ya kupewa nafasi ya kujitetea. Uamuzi wa mwisho wa tuhuma zinazowakabili wajumbe waliochaguliwa na Mkutano Mkuu, utatolewa na Mkutano Mkuu wa Taifa. Kwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji Taifa uamuzi wa mwisho wa tuhuma zinazowakabili utatolewa na Baraza Kuu.

## 18.6 Mapato ya Chama

Chama kitaendesha shughuli zake kutokana na fedha iliyotokana na kiingilio, ada ya kila mwezi, michango, misaada kutoka kwa wafadhili/wahisani na vyama rafiki, miradi ya uchumi ya Chama, Taasisi, watu binafsi na Fedha hizo zitatumika kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Chama.

## 18.7 Mikopo ya Kuendeshea Shughuli za Chama.

Bila kuathiri kifungu chochote cha Katiba hii, Chama kinaweza kukopa ili kuendesha shughuli zake, ikiwemo uwekezaji ili kuboresha huduma za Chama.

## 18.8 Kanuni za Fedha

Kwa mujibu wa Katiba hii, kutakuwepo na Kanuni za Fedha (Financial Regulations) za Chama, ambazo zitaongoza namna ya kusimamia, kutunza na matumizi ya mali na fedha za Chama.

## 18.9 Ukaguzi wa Fedha na Mali

18.9.1 Hesabu za Fedha na Mali za Chama zitakaguliwa kila mwisho wa mwaka wa fedha na Mkaguzi wa Nje anayetambulika na kuidhinishwa na Baraza Kuu kama itakavyowakilishwa na Kamati ya Utendaji.

18.9.2 Taarifa ya ukaguzi wa fedha na mali za Chama zitawasilishwa kwenye kikao cha Baraza Kuu.

## 18.10 Utunzaji wa Kumbukumbu za Chama

Mihutasari ya vikao vya Chama na Karatasi za Kura zitahifadhiwa kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.

## 18.11 Miundo na Kanuni za Utumishi

Kutakuwepo Miundo na Kanuni za Utumishi ambazo zitaongoza namna ya kusimamia na kutekeleza maslahi na maendeleo ya viongozi na watumishi wa Chama.

## 18.12 Uwakilishi wa Wanachama wa TUICO waliopo Zanzibar

18.12.1 Wanachama wa TUICO wanaofanya kazi Zanzibar kwenye Taasisi zenye Makao Makuu Tanzania Bara, ambazo zina matawi yake Zanzibar, watashirikishwa kwenye kikao cha Baraza Kuu na Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama.

18.12.2 Wanachama hao wanaweza kupata haki hii kwa kuzingatia Katiba ya Chama na taratibu zote za Uchaguzi wa Viongozi na Wawakilishi ndani ya Chama kama itakavyoelekezwa na Ofisi ya Katibu Mkuu.

18.12.3 Mkutano wa Viongozi wa Matawi ya Chama-Zanzibar.

(a) Kutakuwa na Mkutano wa Viongozi wa Matawi ya Chama yaliyopo Zanzibar ambao utawachagua wawakilishi hao. Mkutano huo utaandaliwa, kuitishwa na kusimamiwa na Katibu Mkuu au Mwakilishi wake.

(b) Mkutano wa Viongozi wa Matawi ya Chama yaliyopo Zanzibar utafanya yafuatayo:-

(i) Kuchagua wawakilishi wanne (4) wa Mkutano Mkuu TUICO Taifa,angalau mmoja awe Mwanamke.

(ii) Kuchagua wawakilishi wawili wa Baraza Kuu, angalau mmoja awe Mwanamke.

(c) Wawakilishi watakaochaguliwa na Mkutano wa Viongozi wa Matawi yaliyopo Zanzibar kuwa wajumbe wa Baraza Kuu na Mkutano Mkuu TUICO Taifa, watakuwa na haki zote za wajumbe wa Vikao hivyo.

## 18.13 Sekretarieti ya Chama

Kutakuwa na Sekretarieti ya Chama Makao Makuu, ambayo itaundwa na Katibu Mkuu, Katibu Mkuu Msaidizi, Wakuu wa Sekta, Idara na Vitengo.

18.13.1 Akidi ya vikao vya Sekretarieti ni kuanzia nusu ya Wajumbe.

18.13.2 Katika kutimiza majukumu ya Sekretarieti, vikao vyote vya Sekretarieti vitaongozwa na Mwenyekiti ambaye ni Katibu Mkuu au Katibu Mkuu Msaidizi.

18.13.3 Kutakuwa na Katibu wa Sekretarieti, ambaye atachaguliwa miongoni mwa wajumbe na atafanya kazi zote za Ukatibu kwenye vikao vya Sekretarieti.

18.13.4 Majukumu ya Sekretarieti ni:-

(a) Kuratibu utekelezaji wa maazimio ya vikao vya kikatiba vya ngazi ya Taifa.

(b) Kuratibu utekelezaji wa shughuli za Chama za kila siku, ikiwa ni pamoja na

kutoa ushauri na kusaidia ngazi za Kanda, Mkoa na Matawi, kufanikisha malengo na majukumu ya Chama.

(c) Kuandaa vikao vya Kikatiba vya Kamati ya Utendaji Taifa, Baraza Kuu na Mkutano Mkuu Taifa, pamoja na vikao vya kiutendaji.

(d) Kuratibu na kufuatilia kwa karibu maendeleo, fursa na changamoto za Chama.

(e) Kutekeleza kazi nyingine ambazo Baraza Kuu, Kamati ya Utendaji Taifa na Ofisi ya Katibu Mkuu itaelekeza kwa manufaa na ustawi wa Chama na Wanachama.

(f) Kuratibu Chaguzi mbalimbali za Chama.

(g) Kupokea, kujadili na kushauri kuhusu utekelezaji wa shughuli za Sekta, Idara na Vitengo.

(h) Bila kuathiri masharti ya Katiba hii, endapo kutatokea dharura isiyoweza kuzuilika kwa kutokuwepo kwa mmoja wa watia sahihi wa hundi za Chama, Ofisi ya Katibu Mkuu kupitia Sekretarieti inaweza kumteua na kumthibitisha mtia saini mwingine ili kuepusha kusimama kwa shughuli za Chama.

S.L.P. 5680, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: (0) 22 2866910 / 2866960 | Nukushi +255 (0) 22 2866911
Barua pepe: tuico2004@yahoo.com | Tovuti: www.tuico.or.tz